TANGAZO LA SERIKALI Na. 585 la tarehe 12/7/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

**SHERIA NDOGO**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA ZA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmshauri ya Wilaya ya Mbinga;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokotomawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mhudumu'"maana yake ni mtu anayehudumia wateja katika baa, hoteli na mgahawa;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya watu kuuza na kununua bidhaa;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo hii itajumuisha pia kituo cha kupaki malori na vituo vingine vidogo vidogo vya kupakia na kushusha abiria vya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

4.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika

kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

Utoaji wa stakaba dhi za malipo

7.-(1) Ada au ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, utalipwa kwa Halmashauri au kwa Wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Utakuwa ni wajibu wa kila mlipa ada au ushuru kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3) Utakuwa sio utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Ukusanya ji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1) hapo juu, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Ushuru wa nyumba za kulala wageni

9.-(1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anapaswa kulipa asilimia kumi ya mapato yaliyolipwa na mgeni aliyesajiliwa.

(2) Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atawajibika kuwasilisha ushuru wa nyumba ya kulala wageni kila mwezi kwa Halmashauri ndani ya siku saba tangu kumalizika kwa mwezi wa malipo.

Uteuzi wa Wakala

10.-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Ulipaji wa gharama za kuhifadhi mzigo au chombo kilichokamatwa

12.-(1) Halmashauri itatoza kiasi cha asilimia tano ya thamani ya chombo kilichobeba mzigo kwa kila siku kwa mzigo ulioshikiliwa baada ya kukamatwa ukisafirishwa bila ya kulipa ada au ushuru.

(2) Chombo au mzigo husika usipokuwa umelipiwa kwa muda wa siku saba Halmashauri itauza mzigo au chombo hicho kwa njia ya mnada ili kufidia gharama zake.

Fidia ya gharama za uendesha

13. Endapo anayetakiwa kulipa ada au ushuru atakwepa kulipa, gharama zote ambazo zitakuwa zimetumika na Halmashauri wakati wa kumkamata,

ji wa zoezi.

mkosaji atawajibika kuzilipa.

Makosa na adhabu

14.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;
(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;
(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;
(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri; au
(h) atatumia chombo chochote cha usafiri, kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

I. Ada ya kukodisha Mali za Halmashauri

| Namba | Aina ya Mali | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ukumbi wa Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |
| 2 | Mitambo | Kwa mujibu wa mkataba |
| 3 | Chumba cha biashara | Kwa mujibu wa mkataba |
| 4 | Nyumba ya kuishi (ambayo siyo ya watumishi) | Kwa mujibu wa mkataba |
| 5 | Soko:<br>(i) Kizimba | <br>5,000/= kwa mwezi |
| 6 | Turubai | 50,000/= kwa siku |
| 7 | Vibanda vya Gereji | Kwa Mujibu wa mkataba |

II. Ushuru wa Choo na Bafu

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Choo | 200 kwa huduma |
| 2. | Bafu | 300 kwa huduma |

III. Ada ya Kupima Afya ya Wahudumu

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Kinyozi | 10,000/= | Kwa miezi 6 |
| 2 | Mhudumu wa baa | 10,000/= | Kwa miezi 6 |
| 3 | Mhudumu wa nyumba ya kulala wageni | 10,000/= | Kwa miezi 6 |
| 4 | Msusi | 10,000/= | Kwa miezi 6 |
| 5 | Muuzaji wa vyakula vilivyopikwa au kukaangwa | 10,000/= | Kwa miezi 6 |

IV. Ushuru wa Machijio na Ukaguzi wa Nyama

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha ushuru kwa Shilingi |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa machinjioni:<br>(i) Ng'ombe<br>(ii) Mbuzi<br>(iii) Kondoo<br>(iv) Nguruwe<br>(v) Mfugo mwingine ambae hajatajwa | <br>1,000/=<br>500/=<br>500/=<br>1,000/=<br>500/= |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Ushuru wa ukaguzi wa nyama:<br>(i) Ng'ombe<br>(ii) Mbuzi<br>(iii) Kondoo<br>(iv) Nguruwe<br>(v) Mfugo mwingine ambae hajatajwa | <br>1000<br>800<br>800<br>1000<br>500/= |
| 3 | Ushuru wa mnada<br>(i)Ng'ombe<br>(ii) Mbuzi<br>(iii)Kondoo<br>(iv)Nguruwe<br>(v) Mfugo mwingine ambae hajatajwa | <br>6500/=<br>2,500/=<br>2,500/=<br>2,500/=<br>500/= |

V. Kibali cha Kununua Mazao

| Namba | Aina ya Zao | Kiwango cha Ada kwa shilingi |
|---|---|---|
| 1 | Kahawa | 1,000,000/= kwa msimu |

VI. Leseni ya Kununua na kuuza Mazao

| Namba | Aina ya zao | Kiasi kwa shilingi | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Kahawa | 300,000/= | kwa mwaka |
| 2 | Mazao mchanganyiko | 200,000/= | kwa Mwaka |

VII. Ushuru wa Mazao

| Namba | Aina ya Zao | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 3% ya bei ya kununua |
| 2. | Mchele au mpunga | 3% ya bei ya kununua |
| 3. | Maharage | 3% ya bei ya kununua |
| 4. | Karanga | 3% ya bei ya kununua |
| 5. | Alizeti | 3% ya bei ya kununulia |
| 6. | Miwa | 3% ya bei ya kununulia |
| 7. | Korosho | 3% Mazao ya biashara ya bei ya kununua |
| 8. | Tumbaku | 3% Mazao ya biashara ya bei ya kununua |
| 9. | Kahawa | 3% Mazao ya biashara ya bei ya kununua |
| 10. | Mazao mengine ya chakula na biashara ambayo hayakutajwa | 3% ya bei ya kununulia |

VIII. Ushuru wa Gulio

| Namba | Aina ya bidhaa | Ushuru kwa shilingi | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Nguo za mitumba | 500/= | Kwa siku |
| 2. | Nafaka rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 3. | Madawa asili | 500/= | Kwa siku |
| 4. | Migahawa ndani ya soko | 500/= | Kwa siku |
| 5. | Samaki rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 6. | Mboga za majani | 500/= | Kwa siku |
| 7. | Dagaa rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 8. | Wauza vyungu | 500/= | Kwa siku |
| 9. | Miwa rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 10. | Matunda/ nyanya/ vitunguu | 500/= | Kwa siku |
| 11. | Viatu rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 12. | Bidhaa nyinginezo | 500/= | Kwa siku |
| 13. | Bidhaa nyinginepamoja na mazao ya kilimo ambayo hayajatajwa | 500/= | Kwa siku ya gulio tu |

IX. Ada ya Usajili na Ushuru Wa Mitambo, Mwalo Na Makarasha

| Namba | Aina ya Mtambo | Kiasi kwa shilingi | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | MWALO<br>(i) Usajili | 40,000/= | Mara moja wakati wa usajili |
| | (ii) Ushuru | 200,000/= | Mara moja kwa Mwaka |
| 2 | KARASHA<br>(i) Usajili | 20,000/= | Mara moja wakati wa usajili |
| | (ii) Ada | 100,000/= | Mara moja kwa mwaka |
| 3 | Mawe ya Duara | 1,000/= | Mfuko kwa Mwaka |

X. Ushuru wa Malori ya Makaa ya Mawe

| Namba | Aina ya Gari/ inapokwenda | Ushuru kwa shilingi | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Lori linalosafirisha makaa ya mawe kwenda nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. | 1,000 | Kwa Tani moja |
| 2. | Lori linalosafirisha Makaa ya Mawe kutoka | 200/= | Kwa Tani moja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | machimboni kwenda Bandari Kavu (kituo cha Mauzo) | | |

XI. Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni

| Namba | Aina ya Ushuru | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa Nyumba ya Kulala Wageni | Asilimia 10% ya mauzo ya chumba kwa siku |

XII. Ada ya vibali vya ujenzi

| Namba. | Aina ya ujenzi | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | kiwanja cha makazi | 20,000/= kwa ujenzi wa nyumba moja na inayoongezeka italipiwa |
| | Makazi na Biashara | 30,000/= |
| 2. | Taasisi Mbalimbali | 150,000/= |
| 3. | Kiwanda kikubwa | 150,000/= |
| 4. | Kiwanda kidogo | 50,000/= |
| 5. | Kituo cha mafuta | 500,000/= |
| 6. | Ghorofa 1 | 120,000/= |
| 7. | Ghorofa 2 na kuendelea | 30,000/= kwa kila ghorofa inayoongezeka |
| 8. | Kusimika mnara wa mawasiliano ya Simu | 1,500,000/= |
| 9. | Kusimika mnara wa Redio | 1,500,000/= |
| 10. | Ghala au bohari | 200,000/= |
| 11 | Sehemu ya kuoshea magari | 30,000/= |
| 12. | Ujenzi wa Hoteli | 250,000/= |
| 13. | Kibali cha ukarabati wa jengo | 20,000/= |
| 14. | Majengo mengine yote ambayo hayakutajwa | 20,000/= |
| 15 | Uthamini wa jengo | 10% ya thamani ya jengo |

XIII. Ada ya Kubadilisha Matumizi ya Ardhi, Kugawa Viwanja, Mashamba au Kuboresha Mchoro

| Namba | Matumizi ya Awali | Matumizi Yanayoombwa | Kiasi kwa shilingi |
|---|---|---|---|
| 1 | Makazi pekee | Makazi na biashara | 50,000/= |
| 2 | Makazi pekee | Makazi zaidi ya moja | 50,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Makazi pekee | Shule au Hosteli au Zahanati au huduma zingine za jamii | 50,000/= |
| 4 | Makazi pekee | Hoteli | 150,000/= |
| 5 | Makazi na biashara | Kituo cha mafuta | 500,000/= |
| 6 | Makazi na biashara | Maduka makubwa (Super Market au Shopping Mall) | 200,000/= |
| 7 | Makazi pekee | Viwanda au huduma (Service Trade au Industrial) | 200,000/= |
| 8 | Makazi pekee | Ghala (Yard au Godown) | 100,000/= |
| 9 | Biashara | Makazi | 20,000/= |
| 10 | Shamba | Makazi | 50,000/= |
| 11 | Kugawa kiwanja cha Makazi | Makazi | 50,000/= |
| 12 | Kiwanja cha matumizi ya hoteli | Biashara | 200,000/= |

XIV. Ada ya Kuchangia huduma za Ardhi

| Namba | Aina ya Ada | Kiwango cha Ada kwa shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Upimaji wa Ardhi | 50,000/= |
| 2. | Ada ya maombi ya kiwanja | 5,000/= |

XV. Ada na Ushuru wa Mashamba ya Mbegu

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada ya Usajili (Shilingi) | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| | Shamba la Mbegu | 50,000/= kwa mwaka | 2% ya bei ya kuuzia mbegu kwa kilo |

XVI. Ushuru wa Kuegesha Magari Yanayoingia Katika Magulio, Masoko na Minada.

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) kwa Siku |
|---|---|---|
| 1. | Gari au basi kubwa | 2,000/= |
| 2. | Magari madogo (hiace) | 1,000/= |
| 3. | Teksi | 500/= |
| 4. | Pikipiki | 500/= |
| 5. | Bajaji au guta | 1,000/= |
| 6. | Gari binafsi lisilo la biashara | 1,000/= |
| 7. | Gari ya mzigo aina ya Fusso | 2,000/= |
| 8. | Gari la mizigo aina ya Semi Trela | 2,000/= |
| 9. | Gari ya mzigo aina ya kenta | 2,000/= |

XVII. Ada za Vibali vya Burudani

| Namba | Aina ya kibali | Kiwango kwa shilingi | Idadi |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Kibali cha Ligi cha Michezo mbalimbali | 20,000/= | Kwa Ligi |
| 2. | Kibali cha sherehe<br>(i) sherehe kubwa | 10,000/= | Kwa sherehe |
| | (ii) sherehe ndogo | 5,000/= | |
| 3. | Kibali cha tamasha la Ngoma za Asili | 20,000/= | Kwa siku mbili |

XVIII. Ushuru wa Stendi ya basi

| Namba | Aina ya Gari | Kiwango cha Ushuru kwa shilingi | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Basi au lori | 2,000/= | Kwa siku |
| 2. | Hiace | 1,000/= | Kwa siku |
| 3. | Teksi | 500/= | Kwa siku |
| 4. | Bajaji | 500/= | Kwa siku |
| 5. | Bodaboda | 200/= | Kwa siku |
| 6. | Noah | 1,000/= | Kwa siku |
| 7. | Mtu anaeingia stendi | 300/= | |

XIX. Ushuru wa Huduma

| Namba | Aina ya ushuru | Kiasi kwa Shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Huduma | 0.3 % |

XX. Ushuru wa Mazao ya Misitu

| Namba. | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Aina zote za mazao ya misitu isipokuwa mitiki. | Asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia |
| 2. | Mbao laini (saiplas au misindano) | 200/= kwa kila ubao |
| 3. | Mbao laini (mwembe, mnazi, Sederela) | 200/= kwa kila ubao |
| 4. | Mkaa gunia | 1,000/= kwa kila gunia |
| 5. | mbao za miti ya asili | 5% ya bei ya kununulia |
| 6. | kusafirisha mabanzi ya mitiki | (a)chini ya tani moja 1,000/=<br>(b)Tani 1 hadi 3 = 3,000/=<br>(c)Tani 4 hadi 7= 5,000/=<br>(d) Zaidi ya Tani 7=10,000/= |
| 7. | Kusajili au kuchakata au kusafirisha biashara ya mazao ya misitu | 50,000/= kwa Mwaka |
| 8. | Kusafirisha kuni | 200/= kwa kubic mita moja |
| 9. | Nta | 300/= kwa kilo |
| 10. | Banzi | 300/= kwa banzi |
| 11. | Vifaa vilivyotengenezwa kwa mbao | (a) shata za milango mmoja 6,000/=<br>(b) fremu za milango mmoja 5,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | | (c) viti au stuli mmoja 1,000/=<br>(d) kitanda kimoja 6,000/=<br>(e) seti ya makochi 15,000/=<br>(f) kikapu au mkeka 200/= |
| 12. | Mashine ya kuchakata mbao | 50,000/= |
| 13. | Tiba asili au dawa za asili | 10,000/= |
| 14. | Asali | 300/= kwa lita moja |

XXI. Usajili, Kibali na Ushuru wa Matangazo ya Biashara kwa njia ya Vipaza Sauti, Wapiga Mziki, Waonesha Video Au Sinema

| Namba | Aina ya Kibali | Kiasi kwa shilingi | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1 | Kibali cha matangazo ya biashara binafsi | 20,000/= | Kila tangazo |
| 2 | Kibali cha matangazo ya biashara kampuni au taasisi | 50,000/= | Kila tangazo |
| 2 | Usajili wa waonyesha video au sinema | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Usajili wa wapiga muziki | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Kibali cha kupiga mziki kwa wenye vyombo vya muziki | 10,000/= | Kwa kila tukio |
| 5 | Kibali cha kupiga mziki kwa wenye vyombo vya muziki kutoka nje ya Halmashauri | 20,000/= | Kwa kila tukio |

XXII. Ada ya Ukaguzi

| Namba | Aina ya Ukaguzi | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Baa | 15,000/= kwa Mwaka |
| 2 | Mgahawa | 5,000/= kwa Mwaka |
| 3 | Nyumba ya kulala wageni | 15,000/= kwa Mwaka |
| 4 | Gereji | 15,000/= kwa Mwaka |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ..........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya.......................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwamba Tarehe ..........ya Mwezi ................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya …….. ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga za Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi ……………………………………………………………………. badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: ....................................................
Saini: ...................................................

MBELE YA:
Jina……...............................................
Wadhifa: .................................................
Saini: .................................................
Tarehe: ..............................................

Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imegongwa kwenye kanuni hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya mbinga

JOSEPH KASHUSHURA RWIZA,
*Mkurungenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*MBINGA*

DESDERIUS HAULE,
*Mwenyekiti*,
*Halmashauri ya Wilaya,*
*MBINGA*

**NAKUBALI**,

L.S

Dodoma,
20 Juni, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*